
**MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA MAENEO YA KASKAZINI MWA MKOA WA KIGOMA**
**Umetolewa: (22/08/2024)**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2024; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2024 kwa maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

*(i). Kwa ujumla mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.*
*(ii). Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba, 2024.*
*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Disemba, 2024.*
*(iv). Vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2024**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya wilaya za kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Msimu unatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

***Angalizo:***


*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA WILAYA YA KAKONKO
## Umetolewa: 22/08/2024

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2024; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kakonko.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2024 kwa wilaya ya Kakonko, Kigoma.

### Dondoo muhimu

*(i). Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kakonko.*

*(ii). Mvua zitaanza wiki ya nne ya Septemba, 2024 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.*

*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya Disemba, 2024.*

*(iv). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2024 kwa wilaya ya Kakonko

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Septemba, 2024.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu na ya nne ya Disemba, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kakonko ni kati ya milimita 380 hadi 400.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2024.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2024.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu wa udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.

(ii). Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.

(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.

(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua ili kukabiliana na upungufu wa maji unaotarajiwa.

(iii). Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazo hifadhi unyevunyevu katika udongo.

(iv). Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.


Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA WILAYA YA KIBONDO
**Umetolewa: 22/08/2024**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2024; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kibondo.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2024 kwa wilaya ya Kibondo, Kigoma.

### Dondoo muhimu

*(i). Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kibondo.*

*(ii). Mvua zitaanza wiki ya nne ya Septemba, 2024 na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.*

*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya Disemba, 2024.*

*(iv). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2024 kwa wilaya ya Kibondo

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya Septemba, 2024.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu na ya nne ya Disemba, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kibondo ni kati ya milimita 380 hadi 410.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2024.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2024.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu wa udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.

(ii). Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.

(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.

(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua ili kukabiliana na upungufu wa maji unaotarajiwa.

(iii). Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazo hifadhi unyevunyevu katika udongo.

(iv). Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.



*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727N – 01/2023*